Marafiki wa Afrika Tanzania (MAT)
Baramba Girls' Secondary School
P.O.Box 109 Ngara – Kagera
Tel.No. 0628-02575 6 (Ofisi ya mkuu wa shule)
0692- 470428 (Ofisi ya mkuu wa shule)
0753- 742367 (Ofisi ya uhasibu)
Email: *baramba.sec@gmail.com*
bambaraisaias@gmail.com

Date: _____

Mzazi/Mlezi wa _____

YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BARAMBA.

Ninafurahi kukufahamisha kuwa binti yako_____ amechaguliwa kujiunga na kidato cha _____ katika shule ya Sekondari ya Wasichana Baramba kwa mwaka 2018.

1. **KUFIKA:**
   Shule itafunguliwa tarehe ***08/01/2019*** binti yako anatakiwa kufika shuleni siku ya kufunguwa.Akichelewa mpaka ***08/02/2019***, nafasi yake itatolewa kwa mwingine.
2. **ADA NA MICHANGO KWA MWAKA 2019**

MCHANGANUO WA ADA NA MICHANGO YA SHULE 2019.

NO.	VIPENGELE	KIASI
1	Ada kwa mwaka	950,000/=
2	Fomu ya maombi	10,000/=
3	Usajili	35,000/=
4	Sare ya shule	125,000/=
5	Ukaguzi	1,000/=
6	Vyombo ya chakula	10,000/=
7	Matibabu	50,000/=
8	Tahadhari	20,000/=
9	Rimu ya karatasi	12,000/=
10	Kikao cha wazazi	30,000/=
11	Taaluma	50,000/=
12	Mahafali	15,000/=
13	Godoro	20,000/=
14	Maendeleo ya shule	50,000/=
15	Siku ya utamaduni(Cultural day)	25,000/=
16	Michezo (ngazi ya Cluster,wilaya na Taifa)	30,000/=
17	Ujenzi wa fensi	50,000/=
18	Ziara ya masomo(Study Tour)	50,000/=
19	Kitambulisho	5,000/=

	Jumla kuu	**1,538,000/=**

B: ULIPAJI KWA KILA AWAMU UTAFANYIKA MWANAFUNZI ANAPORIPOTI SHULENI.

AWAMU	JANUARI	APRILI	JULAI	SEPTEMBA	JUMLA
KIASI	384,500/=	384,500/=	384,500/=	384,500/=	1,538,000/=

C: AKAUNTI NAMBA ZA SHULE

a) NMB NGARA 3213500108 Baramba girls' secondary school.
b) CRDB NGARA 0150216670300. Baramba secondary school.

Nenda kwenye tawi lolote lililo karibu na wewe ukalipe, utapewa "**pay – in – slip"** utakayompa mwanafunzi ili akija aikabidhi ofisi ya uhasibu shuleni na kupewa stakabadhi yenye nembo ya shule ambayo ndiyo tu halali kwa malipo ya shule.
ZINGATIA:*Usilete fedha taslimu kwa malipo ya ada na michango haitapokelewa*.

3. MAHITAJI MENGINE YA MWANAFUNZI KUJA NAYO SHULENI NI:

3.1) MASOMO: Daftari kubwa 24, peni 10, penseli 2, seti ya jiometri 1,rula 2, na faili 2 (Flat /box faili) mpya za kutunza kumbukumbu zake.Vifaa hivi vitahakikiwa na mwalimu wa darasa.

3.2) MAHITAJI YA BWENI:

1. Beseni moja na ndoo moja ya lita 20.
2. Taulo 1, sabuni za kuogea na kufulia, mafuta ya kujipaka.
3. Dawa ya meno tyubu kubwa 2 na miswaki 2.
4. Shuka mbili rangi ya pinki na blanketi 1.
5. Kitenge au kanga 1.
6. Neti ya mbu.
7. Nguo za ndani: Chupi 10, Sindilia 3, vifaa vya usafi binafsi (peds always 5)
8. Sanduku imara linalofungwa kuhifadhi mali yake.
9. Nguo za kulalia (night dress)
10. Sare ya viatu vyeusi (ngozi) pea 2 kisigino kifupi na soksi nyeupi jozi 3 ndefu.
11. Jaketi 2 kwa ajili ya baridi lisilokuwa na kofia.
12. Aje na toilet paper (5), kioo na chanuo, uzi na sindano ya mkono, pakti 1 ya nyembe.
13. Aje na bukta nyekundu 1, T-shirt nyekundu na raba pea 1, kwa ajili ya mchezo.
14. Sketi nyeusi ya malinda na T-shirt nyekundu kwa ajili ya vazi la kanisani jumapili.
15. Aje na jembe 1, kotama1.
16. Mfagio1 wa chelewa kwa ajili ya kufagia mazingira ya shule .

NB: Vitahakikiwa na Matron na mwalimu wa bweni.
***Vitu vingine vinapatikana kwenye Duka la Shule:**

4. SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE

Mwanafunzi na mzazi wanapaswa kuzisoma kwa makini sheria na taratibu za shule na kuona zipi zinamhusu mzazi na mwanafunzi. Mara
atakapomaliza kusajiriwa atakabidhiwa sheria hizo za shule na atatakiwa kuzifuata zote kikamilifu.

(i).Kofia, mikufu, heleni, pete, bangili, viatu vya ghorofa na mapambo mengine, ni marufuku kuvaliwa shuleni.

(ii). Ni lazima mwanafunzi avae sare ya shule wakati wa masomo darasani, kutoka nje ya shule na wakati wa mihadhara ya shule.

(iii). Ni shule ya Bweni kila mwanafunzi anapaswa kuwa shuleni na kufuata utaratibu wa shughuli zote tangu alfajiri saa 11:30 hadi saa 4:30 usiku. Kutoka na kwenda nyumbani mwanafunzi anavaa traki suit maalumu ya shule.

(iv). Shule hii haina dini, lakini somo la dini linafundishwa. Kila mwanafunzi kwa dhehebu lake. Mwanafunzi haruhusiwi kubadilisha dini bila ridhaa ya mzazi, vile vile shule itamchukulia hatua kali mwanafunzi yeyote atakayepuuza vipindi vya dini na ibada ya dhehebu lake.

(v).Kila mwanafunzi lazima anyoe nywele vizuri ziweze kuchanwa kwa kitana. kunyoa panki au freshi ya unga haviruhusiwi kabisa.

(vi). Ni marufuku kwa mwanafunzi kupaka wanja, kuweka rangi kucha, kufuga kucha na kujigeuza rangi kwa vipodozi.

(vii).Lugha rasmi za kuongea shuleni zitakuwa kiingereza na kifaransa. Hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa kwa mwanafunzi anayekiuka utaratibu huu

(viii).kufanya mitihani ya muhula ama mitihani ya Taifa.

(ix).Siku ya kufungua/ kuanza shule ,masomo yataanza mara moja. Kwa sababu hii,mzazi anahimizwa kuhakikisha kuwa mwanae anaripoti Shuleni kwa siku iliyopangwa na Shule. Vinginevyo,mwanafunzi atarudishwa nyumbani na kutakiwa kurudi Shuleni na mzazi ili mzazi aweze kutoa maelezo kwa nini mwanae amechelewa kuripoti.

Hatutawajibika kwa namna yoyote ile kwa mwanafunzi atakayechelewa kufika shuleni akakuta wenzake wameshaanza masomo.Mzazi atuandikie barua kutujulisha tarehe na siku kijana anapoanza safari ya kwenda shule. Shule itakutaarifu pia tarehe ya kufika shuleni na tarehe ya kwenda nyumbani.

(x)Vifo: mwanafunzi ataruhusiwa tu kuhudhuria kilio iwapo atakuwa amefiwa na mzazi/mlezi anayetambuliwa shuleni. Vilio vingine vya ndugu/jamaa au marafiki mwanafunzi ataomboleza hapa shuleni. Lengo Ia shule ni kumsaidia kijana asipoteza jamaa pamoja na masomo.

(xi).Likizo:Kutakuwa na likizo ndefu ambazo utajulishwa katika ripoti ya muhula ya mtoto wako. Kutakuwepo likizo fupi katikati ya kila muhula likizo fupi ni haki ya mwanafunzi kwenda nyumbani Shule itakuwa na uamuzi wa kuwabakiza shuleni vijana wa vidato Fulani ili kupewa mafunzo ya ziada.

(xii). Mzazi unaombwa kuwa tayari kuhudhuria au kuitikia wito wa shule,mikutano ya wazazi kushirikiana na uongozi.wa shule kutatua matatizo ya mtoto wako.

(xiii).Chakula: Hutolewa na shule na kuliwa ndani ya bwalo la shule. Hairuhisiwi kumletea chakula cha aina yoyote awapo shuleni. Mzazi/mlezi anayetambulika shuleni ataruhusiwa kumtembelea mwanae mara moja kwa mwezi yaani Jumapili ya mwisho ya kila mwezi. Mwanafunzi hataruhusiwa kutembelewa nje ya utaratibu huo. Mzazi/mlezi ajulishe uongozi wa shule ni akina nani wanapaswa kumtembelea mtoto shuleni.

(xiv). Kitu chochote kisichoruhusiwa shuleni kikikamatika hakitarudishwa.

(xv). Wanaoruhusiwa kutembelea au kumpigia simu mtoto ni wale tu walio ainishwa kwenye **FOMU A**.

(xvi). Mzazi umlete mtoto shuleni siku za kazi na si weekend kabla ya 12.00 jioni.

(xvii). Simu ni sumu kwa mwanafunzi hivyo ni marufuku mwanafunzi kuwa na simu kutumia simu yeyote kuwasiliana na mzazi /mlezi.Mwasiliano ya simu kwa mzazi/mlezi ni kwa idhini ya Mkuu wa shule tu kwa kutumia simu za shule.

(xviii). Nguo fupi haziruhusiwi shuleni.Mwanafunzi,asilete simu ya mkononi wala radio.

(xvix). Mwanafunzi anatakiwa kupanda kidato kwa wastani wa shule ambao ni alama **45** . Asipofikisha wastani atakariri darasa au kushauriwa kutafuta shule nyingine.

(xx) Mzazi /mlezi ni sharti alipe ada kwa wakati uliopangwa na uongozi wa Shule ili kurahisisha uendeshaji wa shughuli za kila siku Shuleni. Iwapo mzazi hatalipa kwa wakati bila sababu maalumu na kwa mawasiliano na ungozi wa Shule,mwanae atarudishwa nyumbani.

(xxi) Mzazi/mlezi anahimizwa kufika shuleni angalau mara nne kwa mwaka kupata taarifa kuhusu taaluma na nidhamu ya mwanae.

(xxii) Mzazi anashauriwa kuhakikisha kuwa anapatia mwanae mahitaji muhimu

(daftari,sabuni,karamu,pocket money nk) ili kumjengea mazingira mazuri ya kujifunza na kusoma.

MKUU WA SHULE (sahihi na mhuri)

FOMU MUHIMU ZA KUJAZWA NA KURUDISHWA SHULENI. TAFADHALI MZAZI HAKIKISHA FOMU ZIFUATAZO ZIMEJAZWA NA WAHUSIKA NA MTOTO AJE NAZO SHULENI NA KUZIKABIDHI KWA MSAJILI WA SHULE SIKU YA KURIPOTI.

FOMU (A)

TAMKO RASMI: (*UTHIBITISHO*)

Mimi_____ (*jina kamili la mzazi/mlezi*)wa mtoto aitwaye_____ Jina kamili la mwanafunzi mtajwa hapo juu asome katika shule ya Sekondari ya wasichana Baramba.

a. Nimekubali nitatimiza matakwa yote ya shule kama nitakavyojulishwa kwa maandishi au na uongozi wa shule.
b. Nitalipa karo kwa muda unaotakiwa ili kuepukana na usumbufu na kumkatiza masomo mwanangu.
c. Nitashirikiana kikamilifu na shule kumlea mwanangu mtajwa ili aweze kuwa raia bora wa Tanzania.
d. Ninaelewa kwamba ***NIDHAMU*** ndiyo msingi mkubwa wa mafanikio katika maisha, hivyo utovu wa nidhamu wa mwanafunzi mtajwa kamwe usivumilike.Nitakubaliana na adhabu atakayoamriwa na uongozi wa shule endapo m-toto wangu atakiuka sheria za kinidhamu na taaluma.
e. Nitakuwa tayari kugharimia uharibifu wowote wa mali ya shule au mali ya mwanafunzi utakaosababishwa na mwanangu mtajwa.
f. Ninamruhusu mwanangu mtajwa ashiriki katika shughuli zote za shule ikiwa ni pamoja na kusoma, kama itakavyoelekezwa na uongozi wa shule.
g. Taja matatizo ambayo tunapaswa kutilia maanani tunapokuwa naye hapa shuleni.

NB: ***Mwanao kama ana matatizo ya kiafya aje na cheti cha Daktari cha kuthibitisha***.

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI _____
KAZI YA MZAZI /MLEZI _____
ANUANI YAKE: _____
TAREHE: _____
SIMU ZA MZAZI/MLEZI_____

WATU WATATU WA KUMTEMBELEA SHULENI:

1. Jina_____mahusiano_____simu_____
2. Jina_____mahusiano_____simu_____
3. Jina_____mahusiano_____simu_____

FOMU (B)

(Fomu hii ijazwe na kusainiwa na mzazi/mlezi na kurejeshwa shuleni)

A. MAELEZO KUHUSU MWANAFUNZI(*andika herufi kubwa*)
   1. Majina 3 ya mwanafunzi _____
   2. Tarehe ya kuzaliwa _____
   3. Dini ya mwanafunzi _____

4. Jina la shule ya msingi na wilaya alipomalizia
   _____
5. Photocopy ya cheti cha kuzaliwa _____

UTAMBULISHO WA MZAZI

A. Jina la baba _____
B. Mahali alipozaliwa_____
   I. Kijiji _____
   II. Wilaya _____
   III. Mkoa _____

C. Ni raia wa Tanzania _____
D. Nambari ya hali ya uraia kama si raia kwa kuzaliwa._____
E. Tarehe_____

   A. Jina la mama_____
   B. Mahali alipozaliwa_____
   I. Kijiji _____
   II. Wilaya _____
   III. Mkoa _____

   Ni raia wa Tanzania _____
   Nambari ya hali ya uraia kama si raia kwa kuzaliwa._____
   Tarehe_____

FOMU (C)

Mheshimiwa Daktari

Hospitali ya: _____

S.L.P _____

YAH: MAOMBI YA KUPIMWA

Tafadhali mpime kwa ukamilifu ndugu _____ ili utujulishe kama afya yake inamruhusu afuate masomo ya sekondari ya shule ya wasichana Baramba secondary school iliyoko wilaya ya ngara mkoa wa kagera.

MAONI YA DAKTARI

Nimethibitisha kwamba ndugu _____ (*jina kamili*) **Anaweza/Hawezi** kufuata masomo ya sekondari katika shule ya wasichana Baramba secondary school iliyoko wilaya ya ngara mkoa wa kagera.

Jina la Daktari _____

Sahihi na muhuri _____

Tarehe _____

MEDICAL EXAMINATION:

General	Result
Eyes Ears Skin(allergy,Skin diseases) Chest (Asthma) Abdomen	

• Spleen • Liver • Kidneys	
Others • Pregnancy • Mental illness	
Limbs-Gaint Any abnormality –specify Blood Bs Hb Blood grouping RBCs morphology VDRL/RPR	
Stools : • Ova • Trophozoits • Larva • Cysts • Other forms	
Urine-Albumin -Sugar -Sedment • Ova • Pus cells • Other	
Others: Date of Examination …… Name of examiner …… Signature: …… Official: ……...	